

Maswali

1. Mbona Paulo alikuwa anapelekwa Roma?
2. Nani alikuwa anamchunga Paulo?
3. Mbona Paulo alimwambia Nahodha kwamba wasisafiri wakati huo?
4. Nahodha alifanya nini?
5. Nini ilifanyika baada ya kusafiri?
6. Dhoruba ilikuwa ya namna gani?
7. Malaika aliambia Paulo nini?
8. Ilipofika usiku wa manane, mabaharia waliambia watu wote eti nini?
9. Nini ilifanyika wakati meli ilikaribia nchi kavu?
10. Watu wote walifika namna gani ukingoni salama?

Majibu

1. Paulo alikuwa mfungwa. Alikuwa anapelekwa kuhukumiwa na Kaisari mfalme wa Roma.
2. Akida wa Kirumi alikuwa akimchunga Paulo.
3. Kwa sababu ilikuwa hatari sana kusafiri wakati wa baridi.
4. Nahodha hakusikiliza Paulo. Hewa ilipotulia tu walianza safari.
5. Wimbi ya nguvu ilirusha meli mpaka kwa mchanga ya matope.
6. Upepo ulivuma, kukawa na mawimbi ya nguvu. Hawakuona jua, mwezi wala nyota kwa muda mrefu. Walikuwa wamepotea.
7. Malaika aliambia Paulo kwamba kila mtu aliyekuwa kwa meli atakuwa salama.
8. Mabaharia walisema kwamba walikuwa karibu na ukingo.
9. Meli iligonga na kuingia ndani ya mchanga ya ukingo na ikavunjika kwa vipande.
10. Kuna wenye waliogelea na wengine walin'ginia kwa vipande vya mbao mpaka n'gambo.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



51 Paulo na kuvunjika kwa meli

52

Marejeo

Matendo ya Mitume 27: 9 – 44

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo alikuwa na imani kuu kwa Mungu hata kama alikuwa kwa shida nyingi.

Maneno maalum


- 51.1 Paulo + mfungwa + Roma + meli + hatari + Nahodha + hawakusikiliza + n'goa nanga
- 51.2 Upepo wa nguvu + mchanga wa matope + ogopa + upepo kubwa + dhoruba kubwa + siku nyingi + poteza
- 51.3 Malaika + Paulo + msiogope + yote itakuwa sawa + kula chakula + usiku wa manane + baharia + karibu na ukingo + nanga 4
- 51.4 Pambazuka + ona nchi + meli + konga ukingo wa mchanga + vunjika + ruka ndani ya bahari + ogelea + shikilia vipande vya mbao + wote salama

51.1 Paulo alikuwa mfungwa. Alikuwa anapelekwa Roma ili ahukumiwe mbele ya Kaisari Mfalme mkuu. Kwenda kwa meli ilikuwa safari ndefu sana kutoka kwa nchi ya Israeli mpaka Roma kule Italia. Akida wa Kirumi alikuwa akichunga Paulo.

Ilikuwa mwisho wa Mwaka wakati meli ya Paulo ilin'goa nanga. Meli iliendelea mpaka kisiwa cha Krete, ingawaje hali ya anga ilikuwa

 mbaya, ya dhoruba.

Ilikuwa mbaya sana kusafiri kwa meli wakati hewa ilikuwa ya baridi. Paulo aliambia nahodha wa meli kwamba wakae Krete mpaka wakati baridi imeisha. Lakini nahodha hakusikiliza Paulo. Hali ilipokuwa kama imetulia kidogo, walin'goa nanga na kuendelea.



51.2 Kwa mara moja kulitokea upepo wa nguvu na ukasukuma meli upande wa Kaskazini mwa Afrika kwa mchanga wa matope. Watu waliokuwa kwa meli waliogopa walipoona meli ikirushwa juu na chini kwenye mawimbi ya nguvu. Baharia walipunguza mizigo yao kwa kutupa baadhi ya mizigo baharini ili meli iwe nyepesi. Upopo uliendelea kuvuma usiku na mchana na mawimbi ya nguvu yaligonga meli. Anga ilijaa mawingu meusi na hawakuona jua wala mwezi wala nyota kwa siku nyingi. Walikuwa wamepotea kabisa, wakafkiria kwamba wote watazama kwa hiyo dhoruba.




51.3 Lakini siku moja malaika wa Mungu akaja kwa Paulo na akamwambia, "Usiogope, Paulo. Meli itagwama kwa kisiwa fulani. Lakini wewe na watu wote mlioko kwa meli mtatoka wazima."

Paulo alipoambia kila mtu maneno ya malaika, walifurahi sana. Walikuwa wamekuwa na uoga sana na kwa siku kumi na nne hawakuwa wamekula chakula cho chote. Paulo aliwambia wakule chakula kwa sababu wamejua kwamba wako salama.

Ilipofika usiku wa manane, mabaharia walikundua wako wanakaribia ukingo wa bahari. Meli ilikuwa bado inaendeshwa kwa upopo mkali. Waliweka nje ya meli nanga nne, ili ishikilie meli imara. Walingoja kupambazuke ili waone hiyo nchi.

51.4 Mwishowe kulipambazuka na mwangaza ukawa angani. Waliona kwamba wako karibu na nchi kavu. Waliweza kuona ukingo, lakini walipoendelea, meli iliingia ndani ya mchang'a. Mawimbi mazito yalipiga meli na ikaanza kuvunjika kwa vipande.



Watu waliojua kuogelea waliruka ndani ya bahari na kuogelea mpaka kando. Wengine walitumia vipande vya mbao vilivyovunjika kwa kunin'ginia mpaka n'gambo. Kwa hivyo wote walivuka salama. Mungu alimsaidia Paulo hata kwa hiyo dhoruba kubwa.